# TOFAUTI MUHIMU KATI YA UKRISTO WA BIBLIA NA UKRISTO WA UWONGO (HUMANISM – UTU)

29:9 Shikeni basi ***maneno ya <u>agano</u> hili***, myafanye, ***ili mfanikiwe katika yote mfanyayo***.
Kumb. 29:9

18:1 … Katika mwaka wa tatu wa Hoshea, mwana wa Ela, mfalme wa Israeli, Hezekia, mwana wa Ahazi, mfalme wa Yuda, alianza kutawala.
18:2 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano alipoanza kutawala; akatawala miaka ishirini na kenda katika Yerusalemu;
18:3 ***Akafanya yaliyo mema machoni pa BWANA***, mfano wa yote aliyoyafanya Daudi, baba yake.
18:4 Aliyaondoa maeneo ya juu, akazibomoa sanamu, akakata na kuziangusha nguzo za Ashera; akaivunja vipande vipande ile nyoka ya shaba aliyoifanya Musa; maana hata siku zile wana wa Israeli walikuwa wakiifukizia uvumba; naye akaiita jina lake Nehushtani
18:5 ***Alimtumaini BWANA***, Mungu wa Israeli; hata baada yake hapakuwa na mfano wake katika wafalme wote wa Yuda, wala katika hao waliomtangulia.
18:6 ***Maana alishikamana na BWANA, hakuacha kumfuata, bali alizishika amri zake BWANA alizomwamuru Musa.***
18:7 ***Naye BWANA akawa pamoja naye, kila alikokwenda alifanikiwa***;
2Wafalme 18:1-7

Kichwa cha fundisho hili kinaweza kukushangaza [sana] ndugu yangu msomaji. Unaweza ukawaza, huyu jamaa anadai kwamba Ukristo halisi hauna ***utu*** ndani yake!? Anatofautisha kati ya Ukristo na ***Utu***!? Na unaweza kushikwa na kichefu-chefu na somo langu hili na ukaacha kusoma somo la leo. Kwa hakika Wakristo wengi wa leo ni waumini wa ***Utu*** au ***Humanism*** ndani ya mioyo yao. Wenyewe wanaamini kwamba wao ni Wakristo halisi. Hii ni kwa sababu ***Utu*** uliingizwa taratibu na kwa ujanja mkubwa ndani ya Ukristo, na sasa umeshika mizizi imara. Lakini mimi nakusihi, ndugu yangu, nivumilie kidogo; somo hili ni muhimu sana sana, nina nia ya kukudhihirishia kwamba dini aliyoifunua Bwana wetu katika Biblia ni tofauti, na iko mbali kama mbingu na nchi, na hiki kinachoitwa ***Utu*** au ***Humanism***.

Nitaanza kwa mfano kutoka katika 2Sam. 1:1-16. Nakusihi ndugu msomaji, chukua Biblia yako na ufungue sehemu hiyo na ujisomee mwenyewe. Hapo utaona kwamba Daudi anapokea taarifa za kifo cha mfalme Sauli wa Israeli ambaye alimchukia sana yeye (Daudi) na kwa hakika alifanya juhudi kubwa katika kujaribu kumwua. Lakini Mungu alimlinda na kumnusuru Daudi. Katika maeneo mengi ya vitabu kadhaa vya Biblia Mungu anamzungumzia Daudi kwa kumpa wasifu wa “Daudi, mtumishi wangu.” Utakubaliana na mimi kwamba ni watu wachache sana katika Biblia ambao Mungu anawapa sifa hii kubwa ya kuwaita “mtumishi wangu,” kati yao wakiwemo Musa, Kaleb, na wengine wachache. Turejee kwenye dondoo yetu kuu. Daudi anapokea taarifa ya jinsi mfalme *Sauli alivyouwawa na kijana huyu kwa maombi ya Sauli mwenyewe*. Kwa hakika huyu dogo alikuwa anatafuta sifa tu, akifikiri kwamba Daudi ambaye kwa wakati huu ndiye mfalme mpya wa Israeli atampa fadhila fulani. Badala yake, Daudi anatoa amri kwamba kijana huyu auwawe, na askari mmojawapo wa Daudi anamwua dogo yule. Kosa lake, kulingana na Daudi, ni kwamba alithubutu kunyoosha mkono wake dhidi ya “mpakwa mafuta wa BWANA.” Sasa, somo tunalopata hapa ni kwamba kulingana na simulizi ya kijana huyu, yeye alifanya kitendo cha huruma, kwani kama asingemwua, basi Sauli angalikufa kifo cha aibu na fedheha mbele ya adui wa Israeli. Na kwa kweli Sauli alijua hili, hivyo alipozidiwa vitani aliamua kujiua mwenyewe kwa kuuangukia upanga wake (1Sam. 31:3-4). Katika somo letu la leo, kijana huyu ni ***mwenye Utu***, ***ana imani za ki-utu***, kwani angemwua mfalme aliyemwomba afanye hivyo ili aweze kuepa fedheha ya kuuwawa na adui anayedharauliwa. Lakini tunamwona Daudi, “mtumishi wa BWANA” akiwa na

mtazamo tofauti kabisa. Hapa, ***Daudi ni kielelezo cha Mkristo halisi anayelifahamu vyema neno la Mungu***, *na* ***kijana yule ni kielelezo cha Humanist, muumini wa Utu, anayefuata uongozi wa moyo wake mwenyewe***.

Mfano mwingine: Soma Kumb. 21:18-21. Katika Israeli ya kale, mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 16, mjeuri, asiyerekebika, aliyeshindikana, anayekataa kutubu, amri ya Mungu ilisema kijana huyu auawe kwa mawe; baba na mama yake mwenyewe wamshitaki kwa wazee ambao nao watatamka adhabu hii. Soma vizuri mstari wa mwisho: "… ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako …" Msitari huu unanukuliwa na Paulo katika 1Wakor. 5:13 kuhusiana na kuwafukuza waovu [sugu] ndani ya kanisa. Sasa, ***Humanists*** au ***waumini wa Utu***, wa leo hii, ambao wamejazana katika makanisa yetu, wanasemaje kuhusu waovu hawa wa Kumb. 21:18-21 na 1Wakor. 5:13? "Wafanyiwe *counselling!*" Huu ndio ufumbuzi wa tatizo kutoka kwa Humanists, waumini wa Utu. Halafu waovu hao wanaendelea kubaki makanisani!! Na chachu yao ovu inaendelea kuenea makanisani. Hatimaye kanisa linajaa chachu ya waasi na waovu wa aina nyingi nyingine! Kama wana-kanisa hawachukui hatua madhubuti za kurekebisha hali hii, basi mwisho wa yote Bwana Mwenyewe analikataa kanisa la aina hii, analitoa mbele ya uso Wake na analihukumu. Haya yalitokea kwa taifa la Israeli katika karne ya kwanza. Nadhani unaanza kuona tofauti kuu iliyoko kati ya ***Ukristo wa Biblia na Ukristo wa Utu***.

Kuna watu wataniambia, "Mbona Mwana Mpotevu alisamehewa?" Nami nitasema, soma vizuri masimulizi ya Bwana wetu ya Mwana Mpotevu katika Luka 15:11-32. Kijana yule alijirudi, alitubu, akarejea nyumbani kwa baba yake. Aliyatamka maneno yale muhimu sana moyoni mwake: "Nimetenda makosa dhidi yako na dhidi ya Mungu." Huyu kijana wa Kumb. 21:18-31 hafanyi toba, ni jeuri mpaka dakika ya mwisho ya uhai wake.

Tunahitaji mfano mwingine? Bila shaka! Nao ni huu: Soma Hesabu 5:11-31. Hapo tunasoma juu ya mke ambaye mume wake anashuku amepiga misele nje ya ndoa yake au ambaye kwa hakika amefanya hivyo na mume wake anataka kupata uhakika na kumpa nafasi Mungu atoe adhabu juu yake. Mimi sina uhakika na mfano huu; hata hivyo, ninauweka hapa ili kuwapa nafasi Wakristo waujadili katika makanisa na vikundi vyao. Dondoo:

- Je, jambo hili linaendaje katika Agano Jipya ambapo hakuna '***ritual***' za aina hii?
- Je, ni kweli kwamba katika Agano Jipya hatuwezi kufanya '***ritual***' ya namna hii?
- Je, kumekuwa na matukio ya "kuvimba tumbo, kupooza mapaja, na kutozaa" kati ya wanawake? Jibu ni "Ndiyo," mimi nimeona matukio haya, na nina uhakika msomaji wangu umeshuhudia au umesimuliwa mambo haya. Unaitwa ugonjwa wa uvimbe ndani ya kizazi na dawa yake ni kung'oa kizazi na kukitupa, vinginevyo mama huyu atakufa. Mama huyu 'atapona' lakini hatozaa tena. Lakini je, hii ni adhabu ya Mungu dhidi ya wake wanaotenda dhambi hii? Nani anajua!? Kwa sasa mimi sina majibu. Tafadhali jadili!
- Je, madhila haya yameshawahi kumsibu mwanamke ambaye 'hajamjua mume'? Mimi sijui. Jadili.

Je, kanisa la leo lililojaa 'matunda ya Utu' linafanyaje kuhusiana na suala linalozungumziwa na Mungu wetu katika Hesabu 5:11-31? Wachungaji na wazee wa kanisa, hili linawahusu. Mtupatie majibu.

Mfano mwingine. Na huu ni mfano mkubwa sana, muhimu kweli kweli! Soma Kumbukumbu la Torati, Sura ya 28:1-14; 15-68. Soma Walawi 26:3-13; 14-46. Halafu unaposoma, linganisha na maisha ya Wakristo walioko leo hapa duniani: Wakristo mmoja mmoja, na pia nchi mbalimbali. Utafunguka macho yako, hili nakuhakikishia! Ukiwa mtiifu kwa Mungu wako, wewe kama Mkristo

utapata baraka tele, Mungu mwenyewe atakupigania; kama ni taifa, likiwa na idadi kubwa ya Wakristo watiifu, litasitawi katika kila nyanja, ikiwa ni pamoja na kupata viongozi bora – soma kwa makini, utaliona hili!! Kumbuka, neema za Mungu si mali pekee. Kuna afya njema, amani, nk. Soma pia madhila yatakayowakumba Wakristo wabovu na mataifa yenye idadi kubwa ya Wakristo wabovu. Rudia tena na tena kusoma aya hizi, ukimwomba Mungu akuongoze katika uelewa wako. Utashangaa mwenyewe. Ukiweza, soma pia kitabu cha Ayubu, uone madhila yanayomsibu, na haswa sababu yake; na hatma yake mwishoni mwa kitabu hicho. Kama utaelewa somo, utakubaliana na mimi kwamba wewe Mkristo, ukipatwa na madhila makuu kama hayo yaliyoorodheshwa, basi kuna sababu mojawapo kati ya mbili:

- Umemkosea Mungu kwa kukosa utiifu. Sababu hii ndiyo ya kawaida zaidi! Kwa hiyo madhila yanayokukuta, ***ni kosa lako!*** Hili ni fundisho la Biblia; Ukristo wa Kibiblia unafundisha hivyo.
- Mungu anakupima imani yako kama Ayubu alivyopimwa, kama namna mwanadamu mwenye imani kuu anavyoweza kumshinda Shetani licha ya udhaifu wa kimwili alio nao mwanadamu huyu. Utaona jinsi Mungu alivyomrejeshea Ayubu mara dufu ya baraka alizokuwa nazo hapo kabla, baada ya kushinda mtihani wake huu.

Ebu tuijadili hii sababu ya kwanza, kwamba ***madhila yanayokusibu ni kosa lako!*** Tutajadili kwa mtazamo wa hoja yetu kuu: ***Humanistic Christianity vs Biblical Christianity***; ***Ukristo wa Kibiblia unapotofautishwa na Ukristo wa Kiutu!*** Hapo juu, Mungu ameorodhesha neema utakazopewa Naye ikiwa utakuwa Mkristo mtiifu (Katika Agano Jipya, fundisho hili liko hivi: soma Marko 10:28-30). Na halafu ameorodhesha madhila yatakayokusibu ikiwa utakuwa Mkristo mwasi, mwovu, asiyetii. Kinyume na hivyo, Ukristo wa Kiutu unafundisha kwamba ukipatwa madhila, ni kosa la mtu mwingine!! Na ufumbuzi wake? Mkristo wetu huyu mwovu anaenda kwa ‘Mchungaji’ fulani. Na ‘Mchungaji’ wake huyu atamwekea mikono juu ya kichwa chake, au kifuani mwake, Mkristo huyu atapepesuka na kuanguka chini kwa kishindo, halafu ‘Mchungaji’ wake huyu atatamka kwamba ‘pepo wa wahenga wake’ aliyemsababishia madhila yake sasa ‘ameshindwa’ na kuanzia sasa ataondokana na madhila yanayomsibu. Au watu wanaomtakia mabaya sasa hawataweza kumdhuru tena. Mkristo wetu huyu atapewa ‘maji ya upako’ au ‘mishumaa ya upako’ au ‘vitenge vya upako’, nk ambavyo lazima avilipie! Lakini Mungu mwenyewe anasemaje kuhusu ufumbuzi na namna ya kuondokana na madhila yanayomsibu Mkristo huyu? Soma:

Walawi 26:40-42:
Lakini kama watatubu dhambi zao na dhambi za baba zao, udanganyifu wao dhidi yangu na uadui wao kwangu, ambao ulinifanya niwe na uadui nao hata nikawapeleka katika nchi ya adui zao, wakati mioyo yao isiyotahiriwa itanyenyekea na kutubu dhambi yao, nami nitakumbuka agano langu na Yakobo, na agano langu na Isaki, na agano langu na Abrahamu, nami nitaikumbuka nchi.

Huo ndio ufumbuzi wa madhila yanayomsibu Mkristo. Ukiona unapata madhila katika maisha yako, tambua kwamba Bwana ana ghadhabu na wewe, na unapaswa kumrejea Yeye. Hakuna ufumbuzi mwingine. Huyu ‘Mchungaji’ anayekuahidi kwamba ‘maji ya upako’ yataondoa madhila yanayokusibu ni mganga wa kienyeji tu. Achana naye, urudi kwa Mungu wako, basi.

Najua wapo watu watakaodai, “Hayo yaliwahusu Waisraeli wa Agano la Kale pekee, sisi tuko katika Agano Jipya, tunaabudu katika namna tofauti.” Jibu langu kwao ni,

Yoh. 14:15
Mkinipenda mtazishika amri zangu.

Yoh. 14:21
Aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu, nami nitampenda, na kujidhihirisha kwake.

Yoh. 15:10
Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama mimi nilivyozishika amri za Baba yangu, na kukaa katika pendo lake.

1Yoh. 5:30
Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kuzishika amri zake: na amri zake si nzito.

Na matokeo yake ni haya:

Marko 10:28-30:
10:28 Petro akaanza kumwambia, Tazama, sisi tumeacha kila kitu tukakufuata wewe.
10:29 Yesu akajibu, akasema, Amin, nawaambieni, Mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au mke, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, au kwa ajili ya Injili,
10:30 Atapewa mara mia katika maisha ya sasa, nyumba na ndugu wa kiume, na ndugu wa kike, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na mateso; na katika ulimwengu ujao, uzima wa milele.

Somo ni lile lile kama lilivyoandikwa katika Agano la Kale. Ukishika amri Zake, atakupa neema Zake. Ukiasi amri Zake, utapata madhila; mpaka pale utakapotubu.

Kuna wale Wakristo wengine wenye imani katika ***Utu*** wanaokwambia sababu za madhila yako ziko katika ‘ulimwengu wa roho;’ hivyo na wewe unahitaji kuingia katika ulimwengu huu wa roho na wao wanakupa ‘silaha za kiroho’ ili uweze kupambana na hao jamaa waliomo katika ulimwengu huo ili ushinde vita hii. Ndugu yangu, kwa hakika ulimwengu wa roho upo; na adui zetu wamo humo katika ‘ulimwengu wa roho’ kama Paulo anavyosema:

6:10 Hatimaye ndugu zangu, muwe hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake.
6:11 Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kusimama imara dhidi ya hila zote za Shetani.
6:12 Kwa maana vita yetu si dhidi ya damu na nyama, bali tunapigana dhidi ya tawala, dhidi ya mamlaka, dhidi ya nguvu za giza la ulimwengu huu, na dhidi ya majeshi ya pepo waovu [walio] katika ****himaya za angani***.
6:13 Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuhimili katika siku ya uovu, na mkiishafanya yote, mweze [kuendelea] kusimama.
6:14 Simameni imara basi, mkiwa mmejifunga mkanda wa kweli viunoni, na deraya ya haki vifuani,
6:15 Na miguu yenu ikivaa viatu vya utayari wa Injili ya amani;
6:16 Zaidi ya yote twaeni ***ngao ya imani***, na kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.
6:17 Tena jitwalieni chepeo ya wokovu, na upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu;
6:18 ***Mkiomba kwa sala na kusihi kila wakati katika Roho***, mkikesha katika jambo hilo kwa ustahamilivu, kwa ajili ya watakatifu wote,
Waefe. 6:10-18 (Tafsiri kutoka KJB)

Na katika 2Wakor. 10:3-6 (tafsiri kutoka KJB):
10:3 Maana ***ingawa tunaishi katika mwili***, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili.
10:4 Silaha za vita yetu si silaha za kimwili; bali zinawezeshwa na Mungu ili kuangamiza ngome.

10:5 Tunararua ***fikra na kila dhana*** fidhuli inayojiinua dhidi ya ufahamu wa Mungu; na ***tukitwaa mateka fikra zote zipate kumtii Kristo***:
10:6 Na tutakuwa tayari kuadhibu kila tendo la uasi, mara baada ya utiifu wenu kutimia.

Waefe. 2:1-2
2:1 NANYI mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu,
2:2 Ambamo ndani yake mlienenda, kwa kufuata mazoea ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata ****mtawala wa uweza wa anga***, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa uasi.

Soma kwa makini Waefeso 6:12, hati mlazo, nene "… ***himaya za angani*** …" na Waefeso 2:2 "… ***mtawala wa uweza wa anga*** …" Shetani na majeshi yake walipo kwa sasa ndipo hawa watu wanapaita "ulimwengu wa roho". Soma Luka 10:18 na Ufunuo 12:7-9; Shetani hawezi tena kuingia mbele ya kiti cha enzi huko mbinguni, kama alivyokuwa akifanya wakati anamfitini Ayubu (Ayubu 1:6 na Ayubu 2:1). Kwa sasa himaya yao iko angani kuizunguka dunia, ingawa pia wamegawana maeneo hapa duniani ambamo wanafanya ushawishi wao ovu. Hivyo ulimwengu wa roho siyo mbinguni. Ni mahala mahususi huko angani; na ndiyo maana msemo "ulimwengu wa roho" si sahihi sana, una dosari kidogo. Mtume Yohana aliitwa na Mungu awe shahidi katika mashtaka ya Bwana Yesu dhidi ya taifa la Israeli na uasi ambao taifa hili lilikamilisha katika kumkataa Masihi aliyekuja kwa ajili ya taifa hilo. Hili linasimuliwa katika kitabu cha Ufunuo. Manabii Yeremia, Ezekieli, Danieli, Isaya, nk, nao walikuwa mashahidi dhidi ya taifa la Israeli. Hawa wote waliingia kiuhalisia katika ulimwengu wa roho ulioko mbinguni; waliitwa na Mungu mwenyewe ili kutimiza jukumu hilo. Hawakuingia kwa kutaka wenyewe, kama wanavyodai hawa ndugu wa leo.

Sasa, ukisoma nukuu hizo zote 3 hapo juu, utaona kwamba hakuna haja wala ulazima kwa Mkristo kuingia katika huo unaoitwa "ulimwengu wa roho" ili kufanya vita dhidi ya Shetani na majeshi yake. Kwa kifupi, tunapaswa tu kutembea na Bwana kwa ***kuwa katika Roho Mtakatifu katika matendo yetu na mawazo yetu wakati wote***. Kusali na kuomba wakati wote ndio namna ya kushinda vita hii ya kiroho. Hili ni jambo gumu sana kufanikisha kila wakati, lakini hii ndiyo namna tunavyoweza kumshinda Shetani. Hakuna namna nyingine. Nukta. Asikudanganye mtu yeyote kwamba una ulazima wa 'kuingia katika ulimwengu wa roho'. Huo ni upuuzi mtupu.

Kaa mbali na 'Wachungaji' wanaokuahidi 'kusafisha nyota yako,' hao ni wapiga ramli, waganga wa kienyeji. Kaa nao mbali sana, ndugu yangu. Hao watakuingiza katika laana kuu. Njia wanayopita hao inaelekea motoni tu.

***Utu (Humanism)*** una ushawishi mkubwa sana. Ni mtego ambao ni rahisi kuingia ndani yake. Utu ndio dini iliyoasisiwa na Shetani. Ngoja nikupe mfano. Rais mstaafu wa Marekani, B. Obama, yule mwenye asili yake hapa Afrika, ni mfuasi wa ***Utu***. Yeye ni mtu maarufu mpaka leo, katika wakati wake huu wa kustaafu. Na bado ana ushawishi mkubwa duniani. Lakini unajua? ***Huyu bwana alikuwa promota mkuu wa haki za mashoga***! ***Ni promota mkubwa wa haki ya mjamzito kutoa mimba***! ***Ni promota mkuu wa usoshalisti***! Hii si tu kauli yangu. Fanya utafiti wewe mwenyewe, na utahakikisha hili. Pia alitamka mara nyingi kuwa dini zote zinaelekeza watu kwa Mungu! Unayaona madhara ya Utu?! Mfano mwingine ni mwana wa Afrika anayependwa sana duniani kote, Nelson "Madiba" Mandela. Huyu mzee marehemu mheshimiwa sana ndiye aliyeasisi katiba ya Afrika ya Kusini inayotambua haki za mashoga nchini humo. Hii imepelekea katika hali ya kutisha kabisa ambapo mashoga wawili wanaotaka kuoana kisheria sasa wanaweza kufanya hivyo nchini humo. Watu weusi wengi sana nchini humo bado wamo katika umasikini mkubwa; kupata haki ni changamoto; uhalifu nchini humo upo katika kiwango cha juu kupindukia. Nk, nk. Anayesoma na aelewe! Mungu hadhihakiwi. Kamwe!!

Ushawishi mmojawapo wa ***Utu*** uko hivi: Mkristo asiyeijua Biblia anaulizwa swali kama hili, "Kuna ubaya gani ikiwa mwanamke mwenye uwezo / kipaji cha uongozi, akili na elimu ya kutosha akawa Mchungaji wa Kanisa"? Mkristo anayeulizwa swali hili anaweza kuliona swali lenyewe kuwa na jibu rahisi na la moja kwa moja. Hakuna ubaya wowote, ikiwa mwanamke huyo ana sifa zote ambazo Wachungaji wa kiume wanazo. Sivyo? Lakini Biblia ina maoni gani kuhusu wanawake kuwa Wachungaji?

1Tim. 2:12-14:
2:12 Sitoi ruksa kwa mwanamke kufundisha, wala kuwa na mamlaka juu ya mwanamume, bali kuwa katika utulivu.
2:13 Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye.
2:14 Na Adamu hakudanganywa, bali mwanamke alidanganywa na akaingia katika makosa.

Tutizame tena jinsi ***Humanism / Utu*** ulivyo ni kunyume au tofauti kabisa na imani sahihi ya Kikristo. Tumeamriwa kumtii Mungu kwa kufuata amri Zake. Kwa mfano, tumeamriwa kuupiga vita ushoga (Walawi 18:22; 20:13). Mkristo ameambiwa ushoga ni dhambi kuu; katika Kiingreza Mungu anasema dhambi hii ni "abomination – chukizo," neno zito sana; katika taifa la kale la Israeli, mashoga wakikamatwa, iliamriwa na Mungu wauawe. Dhambi hii na adhabu hii haijatenguliwa katika Agano Jipya (hii itajadiliwa katika somo jingine – ibada za Hekalu na dhabihu pekee ndizo zimetenguliwa katika Agano Jipya). Tumefundishwa na Bwana Yesu na mitume kwamba kutii amri ya upendo ndiyo kutimiza Sheria na mafundisho ya manabii (Matt. 22:37-40; War. 13:10; Waga. 5:14). Sasa, wewe Mkristo, ukifanikiwa kupiga vita dhidi ya Ushoga kwa kumfundisha shoga neno la Mungu hata akaacha dhambi yake hii kabisa, utakuwa umetimiza amri ya upendo kwa jirani zako wengine pia ambao kwa kufuata mfano ule wataacha dhambi hiyo pia. Katika Israeli ya Agano la Kale, mashoga waliuawa. Matokeo yake yalikuwa yale yale – washirika wao waliacha kwa kuogopa adhabu hii kali na kumrudia Mungu. Pale jamii au nchi mojawapo itakapofanikiwa kusimika utawala wa Kikristo, sheria hii na nyingine zinapaswa kurejeshwa katika nchi / jamii hiyo] Ukifanikiwa kumrejesha Mkristo mmoja shoga na kuwafanya wengine warejee kwa BWANA utakuwa umefanikiwa kutimiza kiuhalisia kabisa amri ya Mungu ya kumpenda jirani yako, maana jirani yako ni watu wote! (Soma mfano wa Msamaria Mwema Luka 10:30-37). Mfano huu unatumika pia kwa mtoa mimba, mwizi, mwuaji, mzinzi, nk. Ukimrejesha mmojawapo kwa BWANA, basi utakuwa umetimiza amri ya Mungu ya kumpenda jirani yako. Hata kama huoni matokeo chanya ya juhudi zako, wewe endelea kutimiza wajibu wako, basi. ***Ikiwa kila Mkristo atatimiza wajibu wake kwa njia hii, basi … Mungu anaridhika na mwenendo wa watumishi Wake aliowapa amri zake, na matokeo yake ni kama yanavyoorodheshwa katika kitabu cha Kumbukumbu la Torati 28:1-14 na kitabu cha Walawi 26:3-13 – Mungu atawamwagia baraka tele, kwani hiyo ni ahadi Yake mahususi kwa wale wanaomtii.*** Mvua isiponyesha, tukipata viongozi wabovu, njaa, ardhi isiyo na rutuba, vita zikianza, nk, nk, ***Humanists*** au wafuasi wa ***Utu*** wanasingizia mabadiliko ya hali ya hewa, majirani wagomvi, ubepari mamboleo, na visingizio vingine lukuki; lakini sababu halisi ni uasi dhidi ya amri za Mungu. Mkitoa haki kwa mashoga, watoa mimba, na wengine ambao Mungu amewaorodhesha kama waovu dhidi yake, mtapitia laana zote alizoziorodhesha katika Kumb. 28:15-28 na Walawi 26:14-46.

1:28 Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao potovu, wayafanye yasiyofaa;
1:29 Wakijawa na udhalimu wa kila namna, zinaa, uovu, tamaa, na ubaya; wamejawa na husuda, na uuaji, na fitina, na hadaa; na minong'ono;
1:30 Watu wenye kusengenya, wenye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno, wenye kutunga mabaya, wasiowatii wazazi wao,
1:31 Wasio na ufahamu, ***wenye kuvunja maagano***, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema,

1:32 Ambao wakiijua fika hukumu ya Mungu, ya kwamba ***wanaotenda haya wanastahili kifo***, si tu wanaendelea kuyafanya, bali wanakubaliana na hao wanaoyatenda.
War. 1:28-32

***Humanists*** au ***waumini wa Utu*** wanadhani na wanafundisha kwamba hakuna adhabu ya kifo katika Agano Jipya; soma hati-mlazo nene katika aya ya 32 ya nukuu hapa juu. Mtume Paulo anasema wanaotenda hayo ***wanastahili kifo***. Si kifo cha milele kinachozungumziwa hapo; ni kifo hapa duniani! ***Humanism / Utu*** ni uasi dhidi ya Mungu.

NB: Baraka na majanga yanayoorodheshwa katika vitabu hivyo viwili yanawahusu Wakristo mmoja mmoja pia! Tahadhari!
Kaa mbali sana na ***Utu***; kaa mbali sana na ***Humanism***! Usije ukapotea njia katika safari yako ya kwenda kumwona Mungu. Fanya utafiti wako mwenyewe kuhusu mambo haya. Kuwa Mberea; Mungu atakupa thawabu kuu. Usimtegemee Pastor au Padri wako kupita kiasi. Jisomee wewe mwenyewe!

Kimsingi, Ukristo ni AGANO kati ya Mungu na mfuasi Wake. Na agano lina kanuni zake; kuzifuata kanuni za Agano la Mungu ndio Ukristo halisi, na hapo ndipo Mungu anatimiza upande Wake wa Agano, kama anavyoapa katika agano Lake hilo.

Tumalize kwa maneno ya Mungu yaliyonenwa na nabii Samweli kwa mfalme Sauli pale mfalme huyo alipoamua kutotii amri ya Mungu:

1Samweli 15:22-23a:
Je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu
Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana?
Tazama, kutii ni bora kuliko dhabihu,
Na kusikia kuliko mafuta ya beberu la kondoo.
Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi,
Na ukaidi ni kama udhalimu na [kuabudu] vinyago!

Na ***adhabu kali*** aliyopewa Sauli:

Kwa kuwa umelikataa neno la Bwana,
Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme.
1Samweli 15:23b

**SOMO**: ***Agano letu na Mungu ni sisi kuwa watiifu!***

Imeandikwa na Respicius Kilambo Luciani
https://sayuni.co.tz

0679 900814
075 4375474